**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHE. DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA MAADHIMISHO YA SIKU YA POSTA DUNIANI,

**UKUMBI WA JAKAYA KIKWETE, DODOMA**
**9 OKTOBA, 2021.**

Mhe. Job Ndugai (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mhe. Prof. Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania;

Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.) Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;

Mhe. Rahma Kassim Ali (MBW), Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;

Mhe. Antony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;

Waheshimiwa Mawaziri mliopo hapa leo;

Mhe. Moshi Kakoso (Mb) Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu;

Waheshimiwa Wabunge wote mliopo;

Prof. Davis Mwamfupe, Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma;

Dkt. Zainab Chaula, Katibu Mkuu, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;

Makatibu Wakuu na Naibu Katibu Wakuu mliopo;

Dkt. Fatuma Mganga, Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma;

Bw. Mgonya Benedicto, Msajili wa Hazina;

Bodi na Menejimenti ya Shirika la Posta Tanzania;

Bw. Macrice Mbodo, Kaimu Postamasta Mkuu, Shirika la Posta Tanzania;

Wakuu wa Taasisi na Idara mbalimbali mliopo hapa leo;

Waandishi wa Habari;

Mabibi na Mabwana

***JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA…***

Awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kutufikisha siku ya leo tukiwa na afya njema.

**Pili,** napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji (Mb), Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kumualika Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mgeni Rasmi katika tukio hili muhimu. Mheshimiwa Rais alipenda sana kujumuika nanyi, lakini hakuweza kuungana nanyi kutokana na majukumu mengine ya Kitaifa aliyonayo. Hivyo, ilimpendeza akanipa heshima ya kumuwakilisha na anawasalimu sana. Hii ni mara yangu ya kwanza kushiriki nanyi katika maadhimisho haya, hivyo, kwangu mimi ni faraja kubwa sana kuwa sehemu ya washiriki. Vilevile, na kwa umuhimu wa pekee nawashukuru wanachi wote waliojitokeza na kushiriki katika tukio la leo

**Tatu,** napenda nimpongeze Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na timu yake nzima ya Wizara kwa juhudi na usimamizi wa eneo hili muhimu la mawasiliano yakiwemo mawasiliano ya Posta. Kwa muda mfupi tunashuhudia mageuzi makubwa mliyoyafanya ndani ya Shirika la Posta kwa kuleta huduma mbalimbali zinazoakisi matumizi ya teknolojia katika kuwahudumia watanzania. Napenda kuwapongeza pia wadau wa Sekta hii wakiwemo, Mdhibiti wa Sekta, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na wateja kwa ushirikiano tunaoendelea kuuona ukikua na kuimarika kati yenu. Aidha, ninawaomba muendelee na juhudi za kuiboresha na kuibadilisha sekta ya Posta ili iendane na dunia ya sasa na itoe mchango stahiki katika uchumi wa nchi yetu.

***Mheshimiwa Waziri, Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Posta ni mhimili wa mawasiliano wenye historia ndefu katika mifumo ya mawasiliano duniani kote. Tumesikia Mtendaji Mkuu wa Shirika la Posta akitoa historia ya Umoja wa Posta Duniani (UPU) kama taasisi ya Umoja wa Mataifa inayosimamia maendeleo ya posta duniani tena ni taasisi kongwe ambayo imekuwa ikitoa huduma kuanzia mwaka 1874. Ninafurahi kwamba upo uhusiano mkubwa kati ya malengo makuu ya Umoja wa Posta Duniani na malengo yetu ya Dira ya maendeleo 2025 na yale ya Sera ya Taifa ya Posta ya 2003 hususan katika kuwahudumia wananchi.

Aidha, niwakumbushe tu kwamba masuala mengi ya mawasiliano ya Posta yameahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020 - 2025 hususan katika kifungu cha 102. Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inasisitiza umuhimu wa sekta ya

mawasiliano katika kuwezesha sekta nyingine kukua na kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya nchi. Katika miaka mitano iliyopita (2015 – 2020), Serikali iliendelea kuboresha sekta hiyo kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendelea kuweka mazingira bora ya ushindani kwenye sekta ya mawasiliano ili wananchi wengi waweze kumudu gharama za mawasiliano.

***Mheshimiwa Waziri, Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Leo sitazungumzia historia ya huduma hizi za posta kwa undani wake, Mtendaji Mkuu wa Shirika la Posta ametueleza kwa kina na hata wale waliokuwa hawajui posta ilipotokea sasa wanaelewa. Itoshe kusema tu kuwa mawasiliano ya posta ni mawasiliano kongwe na muhimu sana katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Ni mojawapo ya mawasiliano mama yaliyozaa mawasiliano mengine tunayoyashuhudia hivi sasa ulimwenguni kote.

Kwa kadri mabadiliko yanavyoendelea kutokea katika nyanja za mawasiliano, tumeshuhudia posta ikibadilisha namna ya utoaji huduma zake kwa jamii kulingana na mahitaji ya sasa, na ndiyo maana leo hii tunashuhudia hatua ya posta kuwa ya kidijitali na kuweza kuwafikia watu wengi zaidi kwa urahisi.

***Mheshimiwa Waziri, Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Ninatambua juhudi ambazo Wizara pamoja na Menejimenti ya Shirika la Posta Tanzania mnazifanya kuelekea mageuzi mbalimbali ya kiutendaji ndani ya Shirika mkizingatia kikamilifu Sera ya Taifa ya Posta na malengo yaliyomo kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Tunahitaji kuwa na utendaji wenye tija ikiwa ni pamoja na kutumia mtandao mpana wa Shirika la Posta Tanzania ambao una matawi zaidi ya 350 yaliyosambaa nchi nzima, Bara na Visiwani. Matawi haya yanahitaji kuboreshwa na kuimarishwa kwenye mifumo ya kidigitali ili kuwezesha, kurahisisha utendaji na kuchangia kukuza uchumi wetu. Ni muhimu kwamba, Taasisi hii iguse jamii kihuduma, kwa kuwa ilianzishwa kuhakikisha inatoa huduma kwa niaba ya Serikali na kuwahudumia wanachi wote bila kujali mahali walipo.

***Mheshimiwa Waziri, Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Kama tulivyosikia, Shirika la Posta Tanzania linazo huduma mbalimbali ambazo zinatolewa kwa wananchi tena kwa bei nafuu ukilinganisha na watoa huduma wengine. Zipo huduma za barua za kawaida, barua za haraka yaani EMS, huduma za kifedha, vipeto na pia mnahudumia mizigo mikubwa yaani "Post

Cargo". Nimejulishwa pia kuwa Shirika lina mabasi yanayohudumia wananchi kwenye mikoa ya Kusini. Huduma zote hizi katika mabadiliko makubwa ya kiteknolojia ndani ya nchi yetu na duniani kote zinahitaji kuunganishwa na mitandao ya kidigitali ili kukidhi matakwa na matarajio ya wateja na mazingira ya sasa. Posta ya kidijitali kama alivyoeleza Postamasta Mkuu, zinapaswa kuunganisha watu, kuunganisha Serikali na watu, kuunganisha wafanyabiashara na masoko kwenye biashara mtandao, kuunganisha sekta za uchumi ili kugusa jamii mbalimbali na hasa tunapoadhimisha Siku ya Posta Duniani leo tunajua kuwa nchi zote 192 wanachama wa Umoja wa Posta Duniani zinaunganishwa na kutoa huduma katika ofisi zipatazo 670,000 kuhudumia watu wa jamii mbalimbali katika mfumo mmoja.

***Mheshimiwa Waziri, Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Ninafurahi kufahamu kwamba maboresho makubwa yamefanyika katika utendaji wa Shirika la Posta Tanzania na leo tutakabidhi magari makubwa na vyombo vingine vya usafiri kwa ajili ya huduma mbalimbali za usafirishaji na usambazaji. Niwapongeze kwa hatua hii ambayo sasa itaongeza wigo wa utoaji huduma za usafirishaji na usambazaji. Shirika likiwa ni msambazaji mkuu wa Serikali kwenye barua, nyaraka, vipeto, vifurushi na mizigo litaweza kumudu vema kazi hiyo kutokana na kuongezewa nguvu kwa vitendea kazi hivi.

***Mheshimiwa Waziri, Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Kwa mwaka huu siku ya Posta Duniani inaadhimishwa Kimataifa kwa kaulimbiu isemayo "***Ubunifu kwa Posta Endelevu***". Kauli mbiu hii ina maana kuwa biashara mtandao ndiyo mwelekeo wa huduma za posta duniani. Huduma za Posta kwa sasa zinakabiliwa na ushindani mkubwa kutokana na maendeleo ya Teknolojia ya Mawasiliano. Hivyo, ili huduma ziendelee kuwa endelevu, kuna haja ya kuwa wabunifu Zaidi na kukidhi mahitaji ya wateja. Ni lazima twende sawa na mabadiliko ya TEHAMA na mahitaji ya sasa ya Dunia yanataka nini. Hii ndio tafsiri ya kauli mbiu ya Mwaka huu.

Utafiti wa KPMG (2019) na Benki ya Dunia (2004) unaonesha uhusiano kuwa ukuaji wa huduma za posta unachochea Pato la mtu mmoja mmoja (*GDP per capita*) kuongezeka. Hata hivyo, ili kuwa na matokeo haya, utafiti umeainisha vigezo vikuu vitatu. Kwanza, lazima huduma za Posta ziwe za uhakika, yaani kujenga imani kwa wateja, kuzingatia muda na usalama wa vitu vinavyotumwa. Pili, huduma zitolewe kwa ufanisi; yaani kwa gharama nafuu na kwa ubora wa

hali ya juu. Tatu, huduma za Posta zizingatie mahitaji ya soko na maendeleo ya teknolojia.

Tunapoazimisha Siku hii muhimu, hatuna budi kujitathmini kama huduma zetu za Posta zinazingatia vigezo vilivyotajwa. Vilevile, tujipime vizuri kama huduma zetu za Posta zinaendana na maendeleo yaliyofikiwa na nchi yetu ambayo kwa sasa iko katika uchumi wa kati wa chini.

***Mheshimiwa Waziri, Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Ninatambua juhudi ambazo Shirika la Posta Tanzania mnazifanya kuelekea mageuzi mbalimbali ya kiutendaji ndani ya Shirika mkizingatia kikamilifu Sera ya Taifa ya Posta na malengo yaliyomo kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Lakini ziko dosari kadhaa ambazo ni vizuri mkazitazame na kuzirekebisha:

(i) Bado hamjatumia fursa za biashara za nje ya nchi hususan katika ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Africa (SADC). Takwimu zinaonesha huduma za Posta zinachangia chini ya asilimia 0.5 ya fedha za kigeni zinazotokana na mauzo ya huduma nje ya nchi.

(ii) Ongezeni jitihada katika kutangaza huduma zenu ili jamii ipate kuielewa taswira mpya (new brand) ya Shirika la Posta. Nilitembelea tovuti yenu nikakuta kwa sehemu kubwa iko kwa lugha ya kiingereza. Je watanzania wangapi wa kawaida watawaelewa? Nawataka mtumie na lugha yetu ya Kiswahili ili huduma zenu zifahamike.

(iii) Tumieni maadhimisho haya kutangaza huduma zenu ili kurejesha imani ya Watanzania katika huduma za posta. Awali walichoshwa na huduma hafifu za posta (mizigo/barua kuchelewa au kupotea n ahata wizi wa fedha na vifurushi) kwa kifupi watumishi wa posta mlibweteka! Lakini pia maadhimisho haya ni fursa kwa wananchi kujionea wenyewe huduma mbalimbali za Shirika la Posta katika taswira yake mpya. Huduma za Posta za kidijitali zinapaswa sasa kuunganisha Serikali na wananchi, kuunganisha wafanyabiashara na masoko kwenye biashara mtandao na kuunganisha sekta mbalimbali za uchumi.

(iv) Tangu mwaka 1993 tulifungua sekta ya Posta ili kuruhusu kusajili watoa huduma binafsi (private courier operators) ili waongeze ubunifu na ushindani. Ni masikitiko yangu kwamba mageuzi hayo hayajasaidia

kuwaamsha posta kufanya mabadiliko makubwa katika huduma zinazotolewa na Posta kama ilivyotarajiwa. Hii ndiyo sababu hadi leo bado Watanzania wanapendelea kutuma vifurushi na barua kwa njia za mabasi ya abiria au malori binafsi ya mizigo. Ni dhahiri, bado mageuzi zaidi yanahitajika katika eneo hili.

***Mheshimiwa Waziri, Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Nafahamu changamoto zinazowakabili kiutendaji ikiwamo changamoto za kifedha, ukosefu wa vitendea kazi na mpangilio holela wa baadhi ya mitaa yetu. Serikali imeshachukua hatua za mwanzo kwa Shirika la Posta Tanzania kwa kuwapa vitendea kazi vipya ambavyo nitavikabidhi leo. Huduma za posta zinahitaji vitendea kazi madhubuti na vya kutosha. Pamoja na jitihada hizo za Serikali, bado kunahitajika mchango zaidi kutoka kwa wadau mbalimbali ili kuliwezesha Shirika lichukue nafasi yake. Kwa mukhtadha huo, napenda kuwaelekeza yafuatayo:

(i) Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania endeleeni kusimamia Sekta ya Posta nchini kwa karibu zaidi ili iongeze mchango unaotakiwa katika pato la Taifa. Naigiza Bodi ya Shirika la Posta na Menejiment muwe wabunifu zaidi.

(ii) Ushindani wowote ni lazima uwe na masharti na mazingira yaliyo sawa kwa wote wanaoshiriki. Hivyo naagiza watoa huduma za posta binafsi hakikisheni mnakuwa na leseni ya utoaji wa huduma hizo kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania.

(iii) Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ijizatiti zaidi kwenye utafiti wa ukuaji wa teknolojia ili kurahisisha utendaji kazi wa Serikali kwa ujumla.

(iv) Shirika la Posta Tanzania, jengeni uwezo kwa wafanyakazi wa Sekta ya Posta ili wafanye kazi kwa weledi na juhudi kwa manufaa mapana ya Taifa. Aidha, Shirika la Posta Tanzania mjikite kwenye misingi ya kibiashara, muachane na tamaduni hodhi zilizopitwa na wakati.

***Mheshimiwa Waziri, Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Ninapokaribia kuhitimisha Hotuba yangu naomba kusisitiza yafuatayo:

**Kwanza,** mfahamu kuwa Shirika la Posta Tanzania ni mali ya watanzania wote kwani ni taasisi miongoni mwa taasisi zinazoaminika za Serikali. Mafanikio ya Shirika la Posta ni mafanikio ya watanzania wote. Nitoe wito kwa Watanzania wenzangu tujenge tena Imani na Shirika letu kwa kutumia huduma za Posta kwa manufaa yetu wenyewe na Taifa. Aidha, Taasisi na Idara za Serikali nawashauri nanyi mtumie huduma zilizoboreshwa za Shirika hili kwa maendeleo ya nchi yetu.

**Pili,** ni kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19. Napenda kusisitiza kuwa ni muhimu kwetu kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi ya UVIKO 19. Niwaombe sana Wananchi wote kuchukua tahadhari zote zinazotolewa na wataalamu wetu wa afya na pale unapoona dalili ambazo huzielewi wahi kituo cha kutolea huduma za afya kwa uchunguzi na matibabu zaidi. Vilevile, mtakumbuka kuwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 29 Julai 2021 alizindua rasmi kampeni ya chanjo dhidi ya ugonjwa huu. Hivi sasa, chanjo hiyo inapatikana na inasambazwa nchini kote. Nichukue fursa hii kuwaomba Wananchi mkachanje. Ukichanja na ugonjwa huu ukikupata madhara yake ni madogo tofauti na yule ambaye hajachanja kabisa. Nafahamu zipo taarifa kwenye baadhi ya mitandao ya kijamii ambazo zinapotosha. Niwatoe hofu wananchi wote kuwa chanjo hii ni salama na ni hiyari kwani hakuna atakayechanjwa pasipo ridhaa yake.

***Mheshimiwa Waziri, Viongozi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana***

Baada ya maneno haya nawapongeza tena kwa maadhimisho ya Siku ya Posta Duniani na sasa niko tayari kukabidhi magari mapya makubwa matano (5) yenye uwezo wa kubeba tani thelathini kila moja pamoja na magari madogo 13 na pikipiki 20 ambavyo ni vitendea kazi kwa ajili ya kuboresha huduma za usafirishaji za Shirika la Posta Tanzania.

**Mungi Ibariki Tanzani!**
**Mungu Ibariki Afrika!**

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**